# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**102 /3**
**KISWAHILI – FASIHI**
**KARATASI YA 3**
**KIDATO CHA NNE**
**MTIHANI WA MUHULA 2 2026**
**MUDA : SAA 2 ½**

## SEHEMU A: USHAIRI

### 1. Lazima

**Maswali**

a) Tambua aina ya shairi hili.Toa sababu yako. (alama 2)

- *Shairi arudhi. Linafuata sheria za utunzi.*
- *Mfano - kila ubeti una mishororo minne.* ***Kutaja 1, thibitisho 1***

b) Kwa kutoa idhibati tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

- *Mwanafunzi-Lugha unatufundisha*
- *Aliyekuwa mwanafunzi- kwa kunifanya niwe mtu. Kutaja* ***1,mfano 1***

c) Eleza sifa **tatu** za nafsi nenewa katika shairi. (alama 3)

- *Mshauri-anaelekeza a kutoa ukorofi.*
- *Mwenye busara-Busara za kitabu*
- *Mwenye bidii-anafika darasani mapema*
- *Mvumilivu- hachoki hata anapoulizwa maswali mengi.*
- *Mlumbi- kwa kunena hutokwama*
- *Mlezi mwema-aleaye kwa uzuri namba wani ni mwalimu.* ***Za kwanza 3 x 1***

d) Thibitisha kuwa nafsinenewa amefaulu katika jukumu lake. (alama 1)

- *Watu wote mashuhuri walio katika ofisi nzuri ni mkono wa mwalimu.* ***1x1***

e) Kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo tambua bahari za shairi hili. (alama 2)

i) Vipande

- *Mathnawi –mishororo imegawika katika migao miwili ukwapi na utao.*

ii) Vina

- *Ukaraguni-Vina vya kati na vya mwisho vinabadilika katika kila mshororo.* ***2 x1***

f) Fafanua aina **mbili** za toni katika shairi hili. (alama 2)

- *Toni ya shukurani- Nakushukuru mwalimu*
- *Toni ya masikitiko - cha kulipwa ki kidogo hujalipwa vya kutosha*
- *Toni ya kuridhika – Nashukuru mwalimu, hunifanya niwe mtu* ***Za kwanza 2 x 1***

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

g) Kwa kutolea mifano ,fafanua mbinu mshairi alizotumia ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)

- *Inkisari- kifundisha, wanamsha, wasochoka waloiva*
- *Kuboronga sarufi-Kwa tabia nakuchosha-nakuchosha kwa tabia*
- *Mazida-safisafi,nzurinzuri, ndogondogo*
- *Utohozi- wani/namba/ofisi*
- *Tabdila-chaondowa-chaondoa* ***Lazima atoe mifano. Asipotoa atuzwe 0 zozote 2 x 1***

h) Fafanua mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

- *Sitiari/jazanda- Mwalimu ndiyo kiwanda,binadamu malighafi*
- *Maswali balagha-Walipwaje ndogondogo na kaziyo inachosha?*
- *Takriri-nakuchosha, kidogokidogo, safisafi, nzurinzuri, ndogondogo*
- *Kinaya-Mwalimu analipwa pesa kidogo ilhali kazi yake inachosha.*

i) Andika ubeti wa **saba** kwa lugha nathari. (alama 4)

- ✓ *Mwalimu hajalipwa vya kutosha na hastahili kulipwa kidogo kwa kuwa kazi yake inatosha.Anauliza kwa nini mwalimu alipwe mshahara mdogo ilhali kazi yake inachosha.Anaendelea kumshukuru mwalimu kwa kumfanya awe mtu.*

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**Timothy Arege**: *Bembea ya Maisha*

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.**

**(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandi wala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

- ✓ **Nidaa/ siyahi -** Maskini mke wangu!, Kumbe ilikuwa kweli!, Pombe!
- ✓ **Tashihisi** - umemla bila huruma , Kauli yake ninaona imesimama.
- ✓ **Sitiari** - Silesi zetu za maisha
- ✓ **Utohozi** – silesi
- ✓ **Tashbihi** - kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika **,** Umenichezesha kama mwanasesere
- ✓ **Taswira oni** - mafuriko msimu wa masika
- ✓ **Nahau –** nimekata shauri
- ✓ **Ritifaa –** Yona anasema na pombe kana kwamba pombe ilikuwa hai, 'Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu.'
- ✓ **Uzungumzi nafsia –** Yona anajizungumzia mwenyewe
- ✓ **Takriri/urudiaji/uradidi –** mwaka baada ya mwaka, silesi

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

b) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)

**-** *Toni ya majuto- Yona anajutia*

*- Toni ya huzuni/masikitiko- Kumtesa mkeweMaskini mke wangu!* *2x1 =2*

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima. (alama 8)

**Umuhimu wa Yona**

- *Ametumika kukuza maudhui ya udhalimu kwa kumpiga Sara hadi anapoteza fahamu*
- *Kupitia kwake tunajua athari za udaku; kusemwa na majirani kwa kutokuwa na mrithi kunampaunyanyapaana kumfanya kugeukia ulevi (uk.9)*
- *Kielelezo cha wanaume wasiothamini wanawake*
- *Anakuza ubabedume; hakuthamini Neeme, Asna na Salome kwa kuwa wasichana*
- *Ametumika kuendeleza bidii anapokuwa mwalimu. Alikuwa anabeba vitabu kwendakusahihisha nyumbani wakati wa wikendi (uk.62)*
- *Anakuza baadhi ya sifa za Sara (mvumilivu)*
- *Ametumiwa kujenga mtiririko wa vitushi/ploti ya tamthilia kwa kumpiga Sara, kulewa.*
- *Anajenga mtindo wa tamthilia kupitia mbinu ya dhihaka, ritifaa, methali.*
- *Ni kielelezo cha watu wanaotuzwa katika jamii kutokana na kazi yao nzuri – anatuzwa na serikali na wazazi.* *(8x1)*

3.

(a) "Ndiyo inifae nini? Mimi mwenyewe sikuwa mnyonge. Ninajua maana ya bidii. Lakini vilevile ninajua kuwa bidii pekee haifaulishi kila jambo."

(i) Eleza muktadha wa dondoo. (Alama 4)

- ✓ *Msemaji ni Neema.*
- ✓ *Msemewa ni Bunju.*
- ✓ *Wako nyumbani kwao.*
- ✓ *Wanajadiliana kuhusu matokeo ya shule ya Lemi mtoto wao.*

(ii) Eleza sifa nne za msemewa. (Alama 4)

- ➢ *Bunju ni Karimu - Anamwachia Neema mshahara wake autumie atakavyo.*
- ➢ *Bunju ana mtazamo hasi - Licha ya Lemi kuboresha alama zake shuleni, yeye analalamika kuwa ameshuka nafasi darasani.*
- ➢ *Bunju ni mpenda kulalamika - Analalamikia hali ya Lemi kutoamka mapema.*
- ➢ *Bunju ni mwenye dharau - Anamwita Lemi bumbumbu wa kutupwa kwa kuwa ameshuka nafasi darasani.*
- ➢ *Ana bidii - Anawahi kazini mapema ili kuepuka msongamano barabarani.*
- ➢ *Bunju ni mwajibikaji - Anaijengea familia yake nyumba. Alichukua mkopo wa benki kutimiza hilo.*
- ➢ *Ni mlezi mwema - Anawapa wanawe Lemi na Mina malezi bora: anawaelimisha katika shule bora.*
- ➢ *Ana mapenzi ya dhati - Anamnunulia mkewe Neema gari la kibinafsi.*
- ➢ *Ni mtamaduni - Anashikilia kuwa Sara hawezi kulala kwa nyumba yake kwa kuwa ni kinyume na utamaduni.*
- ➢ *Ni mwepesi wa hasira - Anamwambia Neema mkewe kuwa maneno yake yanachosha.*
- ➢ *Ana mlahaka mwema - Ana uhusiano mzuri na Bwana waliyesoma naye shule ya upili na anamsaidia katika jambo fulani.*
- ➢ *Ana moyo wa kusaidia - Anaahidi Neema kumpiga jeki kwa suala la matibabu ya Sara.*
- ➢ *Ni mbabedume - Analalamika kuwa mkewe Neema hataki kuwa chini ya amri.*
- ➢ *Ni mwenye dhihaka - Anatoa kauli ya kumdhihaki Neema kwa kusema, "Umetimiza yote bibie.Tangu mshahara hadi kunipangia la kufanya na mtoto. Bado tu kunipangia kazi za ndani."*
- ➢ *Ni mfariji mwema - Anamfariji Neema anapoanza kulia. Anamwambia asilie mbele ya mumewe.*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(b) "Wala hakuna wapatanao kama sahani na kawa." Kauli hii inadokeza kuwa migororo lazima iwepo katika jamii. Fafanua migogoro iliyojitokeza kwenye Tamthilia ya Bembea ya Maisha. (Alama 12)

i. *Mgogoro wa Sara na Yona kuhusu mapishi. Yona analalamika kuwa hakuna chakula, Sara anaeleza kuwa ugonjwa umemlemea.*
ii. *Mgororo wa Sara na Yona kuhusu kumwita Neema ili ampeleke Sara kwa matibabu. Sara anashikilia kuwa hakuna haja ya kumsumbua, naye Yona anasisitiza kuwa ni wajibu.*
iii. *Mgogoro wa Sara na Yona kuhusu mtoto wa kiume. Yona alimgombeza na kumpiga Sara kwa kutomzalia mtoto mvulana.*
iv. *Mgogoro wa utamaduni na usasa. Neema na Bunju wanatofautiana kuhusu Sara kulala kwao. Neema anashikilia kuwa mila hizo zimepitwa na wakati.*
v. *Mgogoro wa Asna na Sara wa kimtazamo kuhusu umuhimu wa ndoa. Sara na Asna wanatofautiana kuhusu suala la Asna kuolewa. Asna anaona ndoa kama utumwa, ilhali Sara anamshinikiza kuolewa.*
vi. *Mgogoro baina ya Sara na Asna kuhusu Bunju. Asna anamwona Bunju kama mtu bahiri, Sara asisitiza Bunju apewe heshima yake.*
vii. *Mgogoro wa kimawazo wa Yona. Yona anapatwa na vuta nkuvute ya kimawazo kwa sababu ya kusemwa na jamii alipokosa mtoto mvulana.*
viii. *Mgogoro wa Neema na Bunju kuhusu matokeo ya Lemi shuleni.*
ix. *Mgogoro kati ya Yona na nafsi yake. Anajisuta kwa kumtesa Sara na kuapa kuwa angemtunza uzeeni mwake.*
x. *Mgogoro kati ya Yona na nafsi yake. Anakumbuka namna alivyofanya kazi kwa bidi kabla ya kuingilia ulevi uliomfanya afutwe kazi.*
xi. *Mgogoro kati ya Yona na wazee wenzake. Wazee hawa walimshauri amuoe mke ambaye angemzalia mrithi.*
xii. *Mgogoro kati ya Sara na nafsi yake. Aliumia moyo aliposikia Yona akishauriwa amuoe mke mwingine ili amzalie mrithi.*
xiii. *Mgogoro kati ya Bunju na nafsi yake. Bunju ana madeni mengi ambayo yanamkwaza.*
xiv. *Mgogoro kati ya Asna na nafsi yake, binti huyu amesoma ila hana ajira.*
xv. *Mgogoro kati ya Sara na nafsi yake. Ugonjwa wa moyo unamfanya kuhisi kwamba alikuwa karibu kufa. Anadai kuwa akiitwa ataitika.*
xvi. *Mgogoro kati ya utamaduni na usasa. Wahusika wanaunga mikono pande tofauti mfano Bunju hataki Sara alale chumbani mwao ila Neema anashikilia kuwa hayo ni ya kale.*
xvii. *Mgogoro kati ya Yona na wanafunzi. Wanafunzi waliofika shuleni baada yake kufika lazma wangepata adhabu.*
xviii. *Mgogoro kati ya Neema na nafsi yake. Anahisi kuwa hana muda wa kutosha na Lemi.*

## SEHEMU C: RIWAYA

**Clara Momanyi**: *Nguu za Jadi*

***Jibu swali la 4 au 5***

4. Sasa alifahamu fika kwamba mzigo huo kamwe hauchukuliki. Fedheha ikamshika, uso ukamshuka. Sasa mambo yakamtokea puani.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

*i.Ni maelezo ya msimulizi*
*ii.Anamrejelea Chifu Mshabaha*
*iii.Mshabaha alikuwa ametoka ofisini mwa Mangwasha*
*iv.Mshabaha alikuwa ameenda ofisini mwa Mangwasha kuomba mkopo ila Mangwasha akamfukuza.*

4 x 1 = 4

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(b) Fafanua umuhimu wa anayerejelewa katika kujenga riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 6)

i. *Kuendeleza suala la **usaliti** – Chifu Mshabaha anamsaliti rafiki yake, Sagilu kwa kumwambaa kila alipomwona kwa kuwa hakutaka kuwa na uhusiano na majununi.*
ii. *Kuendeleza maudhui ya **ufisadi** – Mshabaha hakulipa ushuru katika biashara zake alipokuwa akifanya kazi kama chifu.*
iii. *Kuendeleza suala la **udhalimu** – Chifu Mshabaha alimdhalilisha Mangwasha kazini. Alimtumia kama tarishi na wakati mwingine kama topasi huku mshahara wake ukiwa wa kijungujiko.*
iv. *Kubainisha maudhui ya **ukabila** – Chifu Mshabaha aliwachukia sana Waketwa. Alikuwa amejaza watu wa kabila la Wakule katika ofisi yake.*
v. *Kuonyesha suala la **mabadiliko** – baada ya Chifu Mshabaha kuachishwa kazi, analazimika kulipa ushuru kinyume na hali ilivyokuwa alipokuwa chifu.*
vi. *Kupitia kwake tunatambua kuwa **Mangwasha ni jasiri** – Mangwasha anamkabili Chifu Mshabaha kwa ujasiri baada ya chifu huyo kumwachisha kazi.*
vii. *Kukuza **ploti** ya riwaya.*
viii. *Ni mfano wa watu **wapyaro** – anasema kuwa Waketwa hawakuwa na akili.*

*Zozote 6 x 1 = 6*

(c) Bainisha mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. (alama 2)

i. *Sitiari - **mzigo** huo kamwe hauchukuliki*
ii. *Uhaishaji/tashihisi - fedheha ikamshika*
iii. *Msemo - uso ukamshuka; mambo yakamtokea puani* *zozote 2 x1 = 2*

(d) "Sasa mambo yakamtokea puani." Onyesha jinsi mambo yalivyomtokea puani msemaji na wahusika wengine riwayani. (alama 8)

i. *Kuachishwa kazi –Chifu Mshabaha anapigwa kalamu na waziri aliyehusika na masuala ya kiutawala kutokana na matokeo duni ya uteuzi wa wajumbe*
ii. *Kulazimishwa kulipa ushuru – baada ya Chifu Mshabaha kuachishwa kazi, analazimishwa kulipa ushuru au biashara zake zifungwe.*
iii. *Kutiwa mbaroni – Sihaba anatiwa mbaroni kutokana na kuwahusisha wasichana wadogo katika biashara ya ukahaba.*
iv. *Kushindwa katika uchaguzi – Mtemi Lesulia anashindwa uchaguzini kutokana na uongozi wake mbaya.*
v. *Kutengwa na marafiki - Mbwashu anamwambaa Mtemi Lesulia baada ya kushindwa katika uchaguzi. Aidha, Mshabaha alimwambaa Sagilu kila alipomwona kwa kuwa hakutaka kuhusiana na majununi.*
vi. *Kurukwa akili – Sagilu anarukwa na akili aliposhindwa katika uteuzi wa chama.*
vii. *Kuzorota kwa afya - afya ya Nanzia ilianza kuzorota tangu aanze kupoteza mali ya umma aliyohodhi*
viii. *Kutoroka nchi yao - inamlazimu Mbwashu kutorokea Ulaya kwa kuchelea kuchukuliwa hatua za kisheria kwa sababu ya maovu aliyoyatenda wakati wa uongozi wa Mtemi Lesulia.*
ix. *Kutengana na wana wao – Sagilu anatengana na mwanawe Mashauri kwa kuwa na uhusiano na Cheiya ambaye alikuwa mpenziwe Mashauri*
x. *Kuvunjika kwa uchumba – Uchumba wa Cheiya na Mashauri unavunjika kutokana na Cheiya kukosa uaminifu*

**Zozote 8 x 1 = 8**

5. (a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo. (alama 8)

Hakujua liliko bahasha ambayo ingemfungulia milango ya heri. Pengine ingemtoa katika maisha yale ya kujikunakuna. Ingemfanya kujua namna atakavyojenga duka jingine na kumwingiza katika pepo ya furaha daima. Haidhuru atakuwa amewaendea kinyume watu wake aliowapenda. Lakini ni lipi lisilowezekana mbele ya pesa?

Kwanza nani angejua amepokea malaki hayo na kwa sababu gani? "Aah, potelea mbali," aliwaza, "Siku hizi kila mtu anazisaka *chapaa*, haijalishi ni kwa njia gani ilimradi maisha yamnyookee."`Kisha alisita na kusema kimoyomoyo, "Utu? Kwani mtu atakula utu. Inafaa mtu ajijenge kwanza kwa njia yoyote ile kisha afikirie

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

masuala ya utu baadaye. Au hata aungame baadaye. Mungu si Athumani. Atamsikiliza na kupokea msamaha wake. Nani asiyeiba au kupokea mlungula siku hizi? Mimi sitakuwa wa kwanza wala wa mwisho."

i. *Tashihisi - bahasha ambayo ingemfungulia milango ya heri*
ii. *Msemo - milango ya heri*
iii. *Taswira mguso - yale ya kujikunakuna*
iv. *Sitiari - maisha yale ya kujikunakuna*
v. *Swali la balagha - Lakini ni lipi lisilowezekana mbele ya pesa?*
vi. *Misimu - chapaa*
vii. *Uzungumzi nafsia – Mrima anajisemea mwenyewe*
viii. *Takriri/uradidi - **Utu**? Kwani mtu atakula **utu***
ix. *Methali - Mungu si Athumani*
x. *Tanakuzi - **wa kwanza** wala **wa mwisho**."*

***Zozote 8 x 1 = 8***

(b) Fafanua jinsi vijana walivyosawiriwa riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 12)

i. *Vijana ni **katili** – kijana mmoja anampiga kumbo mwanamke fulani hadi akaserereka mtaroni. Pia, Ngoswe anashiriki uuzaji wa dawa za kulevya licha ya kufahamu kuwa vijana wengine walipoteza maisha yao kutokana na matumizi ya dawa hizo.*
ii. *Vijana **wamewajibika** – vijana mabarobaro wanajitolea kulinda usalama katika makazi ya Matango baada ya kina Mangwasha kusimika mahema yao. Aidha, Ngoswe anapotambua kuwa Sagilu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Cheiya, anaenda kuripoti kwa Mashauri, rafikiye.*
iii. *Vijana ni **wakarimu** – kuna vijana waliojitolea kumsaidia Mangwasha kukita hema lake karibu na yale ya wenziwe. Aidha, Mashauri alimpa Cheiya kila alichotaka. Alimkodishia nyumba katika mtaa wa Majuu na kumnunulia gari.*
iv. *Vijana wanatumiwa **kuendeleza ufisadi** – Mtemi Lesulia anawapa vijana vifurushi vya pesa ili wahonge watu siku ya zoezi la uchaguzi wa mchujo kwa lengo la kuharibu zoezi la upigaji kura. Aidha, Mashauri alishirikiana na mzazi wake, Sagilu kufisidi vipusa na meno ya ndovu.*
v. *Wanatumiwa **kuvuruga zoezi la upigaji kura** katika vituo vya wapinzani – Lesulia anawaelekeza vijana kwamba walifaa kuvuruga zoezi la upigaji kura katika vituo ambavyo Lonare alikuwa na wafuasi wengi.*
vi. ***Makini** – Ngoswe anatambua kuwa uhusiano kati ya Sagilu na Cheiya haukuwa ule wa baba na bintiye bali ni wa kimapenzi.*
vii. ***Waaminifu** – Ngoswe alikuwa mwaminifu kwa rafikiye Mashauri. Anamripotia Mashauri kuhusu uhusiano wa Sagilu na Cheiya.*
viii. ***Wakware** – Ngoswe aliwastarehesha na kuwabadilisha warembo mbalimbali wa mji kila uchao.*
ix. ***Wapenda anasa** – Ngoswe aliishi katika kasri kubwa peke yake. Aliishi maisha ya fawaishi. Pesa nyingine alizokusanya kutokana na kodi za nyumba za babake alizifuja kwa raha na anasa.*
x. ***Wabadhirifu** – Ngoswe alizifuja kwa anasa pesa nyingine alizopata kutokana na kodi za nyumba za babake.*
xi. ***Wenye bidii** – Mashauri alitia bidii masomoni hadi akahitimu chuoni katika taaluma ya usanifu Majengo.*
xii. ***Wenye mapenzi** – Mashauri na Cheiya walipendana kama ulimi na mate.*
xiii. ***Vibaraka** – Mashauri alitumiwa na Mtemi Lesulia kutekeleza maovu kama vile alitumiwa kubomoa jumba la Lonare kutokana na husuda tu.*
xiv. ***Wapyaro** – Mashauri anamwita Cheiya kiokote.*
xv. ***Wenye heshima** – Mashauri anawaomba msamaha kina Lonare kwa kuwaingilia katika kikao chao.*
xvi. ***Wenye msimamo thabiti** – Mashauri anapoamua kuhama kutoka nyumbani kwao, anafanya hivyo bila kubadilisha nia yake hata anaposhawishiwa na Sagilu, babake.*
xvii. ***Wasaliti** – Cheiya anamsaliti Mashauri, mpenzi wake kwa kuwa na uhusiano na Sagilu, babake Mashauri.*
xviii. ***Wenye tamaa** - Cheiya alianza kutamani vitu asivyoweza kugharamia.*

***Zozote 12 x 1 =** 12*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Winnie Nyaruri Ogenche:** *Sabina*

6. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

“Akili za masomo huna … zinachangamkia barua na mambo ya wanaume tu. Mamako alikuwa vivyo hivyo na unajua kilichomfika. Kweli mtoto wa nyoka ni nyoka!” Yunuke alimfokea. Alikizima kibatari kile na giza kuu likaivaa nyumba. Mwezi mmoja baada ya mtihani kukamilika, Ombati alifika kijijini kwa ajili ya likizo ya mwezi wa Disemba. Alifika nyumbani kufanya maandalizi ya kupeleka Mike katika shule ya upili kwani alikuwa na imani kuwa angepita mtihani. Ombati alikuwa na jingine. Sabina aliwasikia binamu zake waliokuwa katika shule ya upili wakizungumza kuhusu mpango wa baba yao wa kumwoza kwa kijana mmoja mwendesha pikipiki ili apate mahari ambayo dadake Nyaboke hakumpa.

a) Tambua mbinu zozote za lugha ambazo zinajitokeza katika kifungu hiki. (alama 4)

*i) Methali – mtoto wa nyoka ni nyoka*
*ii) Nidaa – mtoto wa nyoka ni nyoka!*
*iii) Uhuishi – giza kuu likaivaa nyumba*
*iv) Taharuki – Ombati alikuwa na jingine – hatuelezwi ni jambo lipi alikuwa nalo hadi baadaye.*
*v) Mdokezo. Akili za masomo huna …*

b) Fafanua maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 5)

*i) Tamaa – Tamaa inamfanya Ombati kutaka kumwoza Sabina bado akiwa mwanafunzi ili apate mahari (mali)*
*ii) Ubinafsi – Ombati kutaka kumwoza Sabina badala ya kumpeleka kidato cha kwanza. Pia anamtaka mwanawe Mike apite mtihani peke yake.*
*iii) Elimu – Sabina na Mike ni wanafunzi, wamefanya mtihani wa darasa la nane, wanangoja matokeo. Pia binamu wengine wa Sabina wako shule ya upili.*
*iv) Malezi – Ombati alifika kijijini kufanya maandalizi ya kumpeleka Mike katika shule ya upili.*
*v) Ndoa za mapenzi – Ombati kutaka kumwoza Sabina*
*vi) Dhuluma – Sabina anasoma kwa kutumia kibatari pia Ombati kupanga kumwoza Sabina bila hiari ni dhuluma.*

c) **Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu**. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame.”

(i) Pambanua aina **nne** za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

a)

- ✓ ***Taswira hisi*** *– Mizizi ya elimu ni michungu*
- ✓ ***Taswira oni*** *- Mtaka cha mvunguni sharti ainame*
- ✓ ***Taswira muonjo*** *– Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu/ matunda yake ni matamu*
- ✓ ***Taswira mwendo*** *- mtaka cha mvunguni sharti ainame*
- ✓ ***Taswira za kijazanda*** *- kuyaonja matunda ya elimu/ matunda yake ni matamu*

*Za kwanza 4X1=4*

(ii) Kwa kutumia hoja <u>saba</u>, Jadili namna suala la dhuluma lilivyoshughulikiwa katika hadithi ya Sabina. (alama 7)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

- ✓ *Sabina kupewa kazi ya kuuza maziwa sokoni asubuhi na mapema.*
- ✓ *Sabina kupewa kazi ya kutapakaza kisonzo shambani.*
- ✓ *Kupewa kazi nyingi za nyumbani; kupika, kuosha hivyo kukosa muda wa kusoma.*
- ✓ *Binamuze Sabina kumzidishia kazi wanapokuja likizoni kwani wanamtuma ovyo ovyo.*
- ✓ *Sabina kutopewa mahitaji ya kimsingi. Alivaa sare iliyojaa viraka vya kila rangi.(uk35)*
- ✓ *Yunuke kumkaripia Sabina huku akimtusi kiokote, mjalaana, baradhuli.*
- ✓ *Yunuke kumchapa Sabina bila hatia eti kwa kuja na barua (ya mwalimu mkuu) na kuchelewa kutoka shuleni.*
- ✓ *Yunuke kumzimia Sabina kibatari anachotumia kusoma (uk39)*
- ✓ *Yunuke kuchochea Sabina dhidi ya mjombake Ombati (uk39)*
- ✓ *Ombati kutaka kumwoza Sabina kwa umri wake mdogo badala ya kumwelimisha kama wanawe.*
- ✓ *Kumbagua Sabina ambapo Ombati anawasomeshea wanawe kwenye shule ya bweni Golden Heart huku akimpeleka Sabina ya kutwa ili amtumikishe.*
- ✓ *Janadume lililofaa kuitwa babake kumkana Nyaboke mchana kweupe na kumwachia Nyaboke malezi yote peke yake.*
- ✓ *Binamuze Sabina hawakupaswa kumsaidia kufanya kazi kwani kufanya hivyo kulikuwa kinyume na amri mfano; Mike kuandamana naye machungani. (uk36)*
- ✓ *Yunuke kumtoneshea sabina kidonda kwa kumkumbusha kuhusu hayati mamake anapotoka shuleni akiwa amechelewa (uk39)*

*(za kwanza saba 7×1)*

**Pauline Kea:***Kila Mchezea Wembe*

**7. a) Changanua tamathali za usemi katika dondoo lifuatalo. (alama 6)**

Sote tulifahamu kuwa pombe ya Mamapima ni haramu. Na wala hatukulazimishwa kwenda kwake. Maji ya kwake tuliyochapa kwa hiari. Swali linalokosesha wengi usingizi ni, "Je, ni vipi tutoe pesa za jasho letu wenyewe kununua mauti? Jambo la starehe ligeuke kuwa maombolezo? Pengine ni uchochole wetu!" Nilikunywa sumu, Emmi. Huo ndio ukweli hasa wa mambo na hapana haja ya kukibatiza kinywaji hiki. Eti moshi, chang'aa, tear gas, sijui nini. Bora kiitwe sumutu! Sumu hiyo imenipofusha, Emmi, na pengine hata ujogoo wangu ishanibwakura. Uchunguzi umedhihirsha kuwa chang'aa yenyewe ilikuwa imetiwa dawa yakuhifadiwa maiti. Maajabu ya dunia hayakomi jamani!Tangu lini mtu kahifadhiwa ali hai? Hivi sisi ni mizuka tu hatustahili kuwa hospitalini bali kuzimu. Mapipa ya Mamapima ya chang'aa nasikia yalisheheni vituko kocho vya kutia tumbo baridi. Si panya wa kuoza, si nyoka wafu, si sodo na nguo za ndani…….

**A.** *Kinaya – i) walifahamu pombe ni haramu lakini waliinywa.*
*ii) mtu kuhifadhiwa akiwa hai.*
*iii) kutoa pesa kununua mauti*
*iv ) wanajiita mizuka wangali hai.*

**B.** *Misemo/nahau – chapa maji/ kutia tumbo baridi.*

**C.** *Jazanda / stiari – sumu, ujogoo*

**D.** *Chuku - hatustahili kuwa hospitalini bali kuzimu*

**E.** *Tabaini – si panya wa kuoza si nyoka wafu si sodo.*

**F.** *Majazi – mamapima*

**G.** *Kejeli – eti moshi, chang'aa, tear gas.*

**H.** *Taswira – taswira ya pombe iliyotiwa panya wa kuoza, nyoka wafu na sodo.* *(6*1=6)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

b). "Kila mchezea wembe hujikata vyanda vyake." Onyesha jinsi wahusika mbalimbali wanavyojikata vyanda vyao. (Alama 14)

*Kuchezea wembe – kufanya mambo bila kujali athari zake. Mfano: anasa kupindukia. Kila mchezea wembe hujikata vyanda vyake. Maana ni kuwa yeyote anayejiingiza kwenye janga, hatimaye janga hilo humuathiri yeye mwenyewe.*

i. *Tembo anachezea pombe mwishowe anakunywa sumu na kuathirika kiafya – kutapika/kufuja damu*
ii. *Tembo anakuwa mlevi na kushtukia amelala na kibibi na kujutia sana hali hiyo-Anji*
iii. *Walevi wanachezea pombe wakilewa na wengine wakamalizia kufa papo hapo. Mfano: moshi*
iv. *Wanaochezea pombe(wembe) wamejipata wakiwa vipofu -Tembo*
v. *Tembo anaanza kuwa mdanganyifu na kuchezea ndoa yake hadi mkewe anamtoroka.*
vi. *Tembo anapuuza maonyo anayopewa na majirani, familia na jamaa zake kuhusu ulevi. Mwishowe anajipata hospitalini.*
vii. *Mamapima ana mchezo wa kuuza pombe haramu kama kawaida yake lakini anashtukia kufungwa jela.*
viii. *Walevi wengine wanajipata wakiwa hali mahututi hospitali baada ya kubugia pombe-Temo na salim*
ix. *Emmi anamdekeza mumewe na kuchukulia ulevi na kuchelewa nyumbani kama vitu vya kawaida. Mwishowe anajuta kukosa bwana. Anabebeshwa mzigo wa kuwalea watoto mwenyewe.*
x. *Kuchezea pombe kunasababisha migogoro katika ndoa- Emmi anadai talaka.*
xi. *Kuchezea pombe kunamgharibu Tembo pesa nyingi. Anaporwa pesa nyingi akiwa mlevi isipokuwa akiba aliyoficha ndani ya soksi ambayo ilimlipa Anji.*
xii. *Kuchezea pombe kunafukarisha kihali na hisia ikisaikoloji. Tembo anajihusisha na unywaji wa pombe haramu ambao hatimaye unamlaza hospitalini. Pombe hii imempofusha, hali chakula au hata kusimama kutoka kitandani. Wapo wahusika wengine walioathirika kwa unywaji wa pombe hii kama vile bwana Salim ambaye wamelazwa pamoja na Tembo hospitali ya uhai ni Neema.*
xiii. *Kabla Tembo hajalazwa hospitalini, hali hii yake ya ulevi ili – mtia kwenye masaibu mengi kama vile; kukosana na wazazi wake, kuzua vurugu siku ya mazishi ya mpwa wake, mtoto wa Natasha. Alijikuta chumba cha Bi – kizee, Anji siku moja ulevi ulipomzidi asiweze kueleza alivyofika pale.*
xiv. *Kufutwa kazi kama Tembo.*
xv. *Kutelekeza familia, Tembo hashughulikii mahitaji ya familia yake kama vile chakula.*
xvi. *Matusi – Tembo anamtusi mkewe Emmi anapolewa.*
xvii. *Kujitia aibu – Tembo anazua rabsha katika mazishi ya mpwa wake.* 14 x 4 = 14

## 8. SEHEMU D : FASIHI SIMULIZI

**<u>Maswali</u>**

**(i)** Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)
- *Ngano ya Usuli – inatueleza kwa nini urafiki wa nyani na mamba ulisambaratika.*

**(ii)** Tambua mbinu sita kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (alama 6)
- *Nahau – kufa kuzikana/Pasulia mbarika*
- *Tashibihi – kufaana kama ndugu wa toka nitoke /kama kupe na mkia wa ng'ombe*
- *Methali – maji hufuata mkondo/ lisilobudi hutendwa*
- *Uhuishi/tashihisi – kuchekelewa na nyavu/njaa kubisha hodi*
- *Mdokezo wa methali – alikuwa mla nawe tu.*
- *Uzuri wako wa mkakasi*
- *Chuku – maghala yakishiba na kutapika*
- *Takriri – alingoja... akangoja... akangoja*
- *Mdokezo – alingoja .... mwaka...*
- *Dayalojia – kati ya nyani na mamba*
- *Balagha – mbona haji kukuona?*
- *Uzungumzaji nafsia – una njaa bwana, familia yako itaangamia.* *(za kwanza 6 x 1 = 6)*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**(iii)** Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo Matano muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (alama 5)

- *Nitahusisha hadhira ili kuundoa ukinaifu*
- *Nitatumia uigizaji – matendo ili kusisitiza ujumbe*
- *Kutumia viziada lugha – ishara za uso, mikono*
- *Kutumia maleba yanayoafikiana na hadithi inayowasilishwa*
- *Kubadilisha toni*
- *kiimbo kulingana na ujumbe ninaopitisha*
- *Kuwa mbaraza, kuingiliana vyema na hadhira yangu.*
- *Kuelewa lugha ya hadhira*
- *Kuwa mkakamavu/jasiri*
- *Kuwa mfaraguzi – kubadilisha hadithi*
- *kuwa mcheshi ili kuchangamsha hadhira yangu.*
- *Kuelewa hadhira yangu na mahitaji yake*
- *Kutumia sauti inayosikika* *(za kwanza 5 x 1 = 5)*

**(iv)** Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. (alama 3)

- *Hueleza chanzo cha hali Fulani m.f chanzo cha uadui kati ya mamba na nyani*
- *Huadilisha – kukashifu tabia hasi kama usaliti*
- *Huburudisha watu wanapotambiwa*
- *Hukuza ubunifu*
- *Huhifadhi na kendeleza utamaduni wa jamii*
- *Hukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani*
- *Hukuza umoja/ushirikiano watu wnapojumuika pamoja kutambiana*
- *Huendeleza historia ya jamii kwa kuvitamba kwa vizazi mbalimbali.*
- *Huelimisha wanajamii kuwepo kwa funzo*
- *Hutumiwa kupitisha muda.* *(zozote 3 x 1 = 3)*

**(v)** Kwa kutoa hoja nne jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. (alama 4)

- *Huashiria mwisho wa utambaji*
- *Humpisha mtambaji anayefuata.*
- *Huitoa hadhira kwenye ulimwengu wa fantasia hadi ulimwengu halisi.*
- *Huwapumzisha/kutuliza hadhira – kwa kutoa suluhisho la mgogoro uliokuwepo katika hadithi.*
- *Hutangaza adili na funzo la ngano.*
- *Huwapa wasikilizaji changamoto ya kuwa watambaji bora.*
- *Hupisha watu kwenye shughuli nyingine.*
- *Hutia watu mshawasha wa kusikiliza hadithi nyingine pengine kupitia taharuki inayoibuliwa na fanani*

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes